

Biblia inasemaje.....

Yesu aliyachukuliaje maandiko?

Sehemu ya nne

“Ibrahimu akasema, wanao Musa na manabii; na wawasikillize wao.” Luka 19:29

“Lakini litimie lile neno lililoandikwa katika torati yao” Yohana 15:25

“Yesu akawajibu, Je haikuandikwa katika torati yenu....na maandiko hayawezi kutanguka” Yohana 10 34-35

Maandiko haya hudhihirisha bila shaka kwamba Yesu aliamini katika uweza na mamlaka iliyo katika Agano la kale. Katika Injili kama ilivyoandikwa na Luka juu ya Tajiri na Lazaro, Yesu alizungumzia utoshelevu wa neno la Mungu. Akimnukuu Ibrahimu, Yesu alisema, “Wanao Musa na manabii; na wawasikilize wao.” Yesu alijua kwamba Wayahudi kama taifa walikuwa na sheria, na ili kumpendeza Mungu walitakiwa kufuata sheria hiyo.

Katika Yohana 15:25, Yesu alinukuu Zaburi 69:4 alipokuwa anaongelea “kilichoandikwa kwenye sheria yao.” Zingatia kwamba Yesu alijua kuwa maneno ya Musa, Mananbii na Mungu ndiyo sheria ambayo Wayahudi waliyotakiwa kuitii, sheria ambayo haikuweza kutanguka (Yohana 10:34-35). Sheria ile isiyoweza kutanguka, inatuongoza kwenda kwa Kristo leo (Wagalatia 3:22-29) Kristo amabaye Baba anatuambia kuwa tumsikilize yeye (Mathayo 17:5). Mungu alimpa Yesu mamlaka yote “mbinguni na duniani” Mathayo 28:18). Kwa mamlaka hii, Yesu alimletea wanadamu maneno ya uzima yavezayo kuokoa na kuhukumu Yohana 12:44-50.

Kama wanadamu, tunatakiwa kutambua kwamba leo kuna mamlaka katika maandiko. Na kama Wayahudi walivyokuwa na sheria yao vivyo hivyo wanandamu wa leo tuna maneno ya Yesu yenyе mamlaka na ndiyo yatakayotuhukumu siku ya mwisho, yakaletwa kwetu na Roho Mtakatifu; na maneno haya hayawezi kutanguka.